# Title I – Sera ya Uhusikaji wa Wazazi na Jamii

Hii Sera na mpango wa kuitekeleza zimeundwa kwa ushirika na pamoja na makubaliano ya, na zitasambazwa kwa, wazazi na jamii za wanafunzi wanaoshiriki kwa mpango wa Title I. Wazazi watajulishwa kuhusu hii sera kwa njia na namna inayoeleweka na ya usawa, kadri ya uwezo, na kwa lugha inayoeleweka na wapokezi. Hii Sera itakuwepo kwa jumuiya na itafafanuliwa na kuimarishwa ili kukidhi mahitaji yanayobadilika ya wazazi, jamii na shule.

**MATARAJIO YA UHUSIKAJI WA WAZAZI NA JAMII** Kwa uzito wa uthibitishaji wa uwepo wa raslimali na habari ingine mwafaka kutoka kwa serikali ya jimbo na ya nchi nzima, ni lengo la Halmashauri/Bodi kuwapa wazazi na jamii za wanafunzi washiriki nafasi za uwazi kushiriki kwa njia zilizopangwa, kwa kuendelea na kwa wakati unaofaa katika vikao vya kupanga, kuratibu, na kuimarisha mpango wa Title I, pamoja na nafasi za kupendekeza mabadiliko, kwa mujibu wa mahitaji yanayobadilika ya wazazi, jamii na shule.

Maoni yote yanayohusu kutoridhika kwa wazazi na jamii kuhusu mpango wa Title I yatakusanywa na kuwasilishwa pamoja na mpango kwa Idara ya Elimu.

Mpango wa Title I utabuniwa kuwsaidia wanafunzi kupata ujuzi na kufikia malengo yaliyowekwa na sheria, pamoja na malengo na viwango vilivyowekwa na Bodi. Haya malengo na viwango vitawasilishwa kwa wazazi na jamii kwa njia itakayowapa haya mambo: (1) habari kuhusu mipango kwa wakati unaofaa; (2) taswira na ufafanuzi wa mtaala wa shule, aina za mitihani ya kimasomo yanayotumiwa kupima mwendeleo wa mwanafunzi, viwango vya matokeo kwa viwango vigumu katika jimbo; kiwango cha matokeo ya mtoto wao katika mitihani migumu ya kimasomo jimboni; na (3) ikiombwa, nafasi za mikutano ya mara kwa mara kujadili mapendekezo na kushiriki katika maamuzi yanayohusu elimu ya watoto wao.

**UHIMILI WA MPANGO** Kama mgao wa Title I wa Wilaya ni $500,000 ama zaidi, Wilaya itaweka kando angalau asilimia moja (1%) ya huo mgao kwa sababu ya kuhadharisha/kutangaza uhusikaji wa wazazi na jamii na itazigawia shule za Title I angalau asilimia tisini (90%) ya fedha zilizohifadhiwa. Shule zilizo na haja kubwa zitakuwa za kwanza kupata msaada. Wazazi na jamii za wanafunzi washiriki zitapata nafasi ya kuamua jinsi hizi fedha za Title I zitakavyotumiwa kwa shughuli za uhusishaji wa wazazi na jamii. Wilaya itasaidia na uratibu, usaidizi wa kiufundi, na usaidizi mwingine mwafaka kudaidia shule kupanga na kutekeleza shughuli mathubuti za

uhusishaji wa wazazi na jamii kuimarisha matokeo ya wanafunzi masomoni na matokeo ya shule. Hivi vipimo vyaweza kujumuisha, pamoja na mengine, haya maneno: 1. Utengaji kando wa raslimali za kusaidia katika kuwasiliana na wazazi na jamii, kuwasafirisha kwenda mikutanoni na/ama matembezi ya nyumbani, huduma za utunzaji wa watoto wakati wa mikutano, kuwahimiza kutumia vituo vya huduma kwa jamii vilivyoko, na kushirikiana nao kuimarisha ujuzi wao kama wazazi, haswa zile zitakaowawezesha kuwasaidia watoto wao kuimarisha matokeo yao ya kielimu. Raslimali zaweza kuwa ni watu binafsi, mashirika, vifaa, na huduma.





**UHIMILI WA MPANGO (KUENDELEA)** 2. Chaguo za kushirikiana, kuratibu na kuunganisha mbinu za mpango wa Title I na huduma

za mipango mingine ya jumuiya, biashara, na mashirika. 3. Utambuzi wa njia ambazo wazazi na jamii wanaweza kuhusishwa kwa shughuli za kuwatayarisha wafanyikazi kuonyesha umuhimu wa kuwahusisha wazazi na jamii na mbinu tofauti zilizoundwa kwa sababu ya kufanikisha uhusikaji wa wazazi na jamii kama wahusika sawa kwa elimu ya watoto wao. 4. Kufanya juhudi ya kufanya mkutano wa mwaka kwa wakati unaowafaa wazazi na jamii za watoto wanaoshiriki ambapo wote watakaribishwa na kuhimizwa kuhudhuria na kuwafahamisha kuhusu ushiriki wa shule yao pamoja na kanuni za mipango ya Title I na haki zao za kushiriki. 5. Kuunda na kutekeleza mpango wa kupima maendeleo ambapo wazazi wanaweza kutoa maoni yao kuhusu maudhui na ufanisi wa hii Sera kuimarisha ubora wa masomo katika shule zinazopokea fedha za Title I, na mpango ulioundwa kuutekeleza. Huu mfumo utafuata hizi hatua: Je, hii Sera inaongeza ushiriki wa wazazi?

Kuna vikwazo vipi vinavyowazuiya wazazi kushiriki, na ni vipi vinaweza kupunguzwa

ama
kuondolewa?

Matokeo ya makadirio ya mwaka yatatumiwa kuunda mbinu za kuimarisha shule

na kurekebisha hii Sera, ikihitajika.

6. Katika kupanga shughuli na vifaa kuhusu wazazi, juhudi za ziada zitachukuliwa kuwafikia na kuwahusisha wale ambao hali zao za kiuchumi ni dhaifu, walemavu, walio na ufasaha duni wa Kiingereza, walio na elimu duni, ama ambao asili yao ni ya uchache.

**SERA YA SHULE** Kila shule itawasilisha kwa Mkurugenzi na Bodi, kwa ukaguzi na kutoa maoni, sera yake ya Title I kuhusu uhusishaji wa wazazi na jamii, ambayo ni lazima ifuate kanuni zote za kisheria, ikiwa ni pamoja na kubaliano baina ya shule na mzazi lililoundwa kwa mujibu wa matakwa ya kisheria. Hii Sera itaundwa kwa ushirika na, na kusambazwa na shule kwa, wazazi wa wanafunzi washiriki. Nakala ya sera ya kila shule ya uhusishaji wa wazazi na jamii pamoja na orodha andamanaji itahifathiwa kwa faili katika Ofisi Kuu.

**MAREJEO:**

Sekemu 1118 ya Sheria ya Kuimarisha Shule za Marekani (IASA) of 1994 P. L. 114-95, (Sheria ya Kila Mwanafunzi Anafanikiwa ya 2015) KRS 157.077; KRS 158.645, KRS 158.6451 KRS 158.865; KRS 158.866; KRS 158.867 20 U.S.C. § 6318; 34 C.F.R. § 200.28





**SERA ANDAMANAJI:**

03.112; 08.1345; 09.11

Zilikubaliwa/Zilibadilishwa: 7/24/2017 # ya Amri: K.2